# UKWELI KUHUSU HOMA YA INI

## Homa ya Ini A

Inasababishwa na Virusi A vya Homa ya Ini (VAH)

Hudumu kwa... **6 miezi**

**Homa ya Ini A huenea kwa:**

- Kula/kunywa vitu vichafu vyenye vimelea vya kinyesi cha binadamu
- Kugusana, kwa mfano, kufanya ngono zembe na mtu mwenye virusi vya Homa ya Ini A
- Kugusa damu ya mtu mwenye virusi vya Homa ya Ini A

**Homa ya Ini A SI tishio sana!**

## Homa ya Ini B

Inasababishwa na Virusi B vya Homa ya Ini (VBH)

Hudumu kwa... **Maisha Yote** kama unaonezeka na kuwa sugu

**Homa ya Ini B huenea kwa:**

- Kugusa damu au majimaji ya mwilini ya mwenye virusi vya Homa ya Ini B
- Kufanya ngono zembe (bila kondomu) na mtu mwenye Homa ya Ini B
- Kuambukiza kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito au wakati wa kujifungua

**Homa ya Ini B INAWEZA kuwa tishio!**

## Homa ya Ini C

Inasababishwa na Virusi C vya Homa ya Ini (VCH)

Hudumu kwa... **Maisha Yote** kama unaonezeka na kuwa sugu

**Homa ya Ini C huenea kwa:**

- Kugusa damu ya mtu mwenye Homa ya Ini C
- Kufanya ngono zembe (bila kondomu) na mtu mwenye Homa ya Ini C
- Kuambukiza kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito au wakati wa kujifungua

**Homa ya Ini C INAWEZA kuwa tishio!**

## JE, TIBA IPO?

**HAPANA**

kwa sasa tiba ipo

**NDIYO!**

kuzuia ugonjwa usiongezeke lakini hakuna tiba

**NDIYO!**

zaidi ya 95% ya watu wamefanikiwa kutibu kwa kumeza kidonge 1-3 kwa siku, kwa miezi 2-3

**Dalili zinatofautiana, unaweza usione ama ukaona moja au zaidi ya zifuatazo...**

- ngozi au macho kuwa ya njano (homa ya manjano)
- maumivu ya tumbo
- kichefuchefu au kutapika
- uchovu
- homa
- kukosa hamu ya kula
- mkojo mweusi, kinyesi cha kahawia, au kuharisha

## NJIA ZA KUJIKINGA NI ZIPI?

### PATA CHANJO!

- Nawa mikono kwa maji safi na sabuni mara baada ya kutoka uani, na kabla ya kuandaa au kula chakula
- Tumia kondomu mara kwa mara na kwa usahihi wakati wa tendo la ndoa

### PATA CHANJO!

- Usitumie vitu vyenye damu ya mwingine, kwa mfano sindano au vifaa vingine vinavyotumika kuandaa, kuchomea, au kujidungia madawa ya kulevya
- Tumia kondomu mara kwa mara na kwa usahihi wakati wa tendo la ndoa
- Epuka kuchora tatuu kiholela au kujitoga

### CHANJO HAIPO!

- Usitumie vitu vyenye damu ya mwingine, kwa mfano sindano au vifaa vingine vinavyotumika kuandaa, kuchomea, au kujidungia madawa ya kulevya
- Tumia kondomu mara kwa mara na kwa usahihi wakati wa tendo la ndoa
- Epuka uchoraji tatuu kiholela au kujitoga

END THE SYNDEMIC TENNESSEE

**Fahamu ikiwa una homa ya ini A, B, au C kwa kupima damu!**

Dept. of Health, Authorization # MX2KH6-1, electronic only, June 6, 2025. This public document was promulgated at a cost of $Electronic per copy.